

**Sikiliza na Ujifunze - Mazingira**

**05 – Firewood ( Kuni )**

**Text: Richard Lough**

**Redaktion und Idee: Johannes Beck**

**Translator: Mohamed Dahman**

---

Hujambo msikilizaji! Karibu katika mfululizo wa vipindi maalum vya Sikiliza na Ujifunze kuhusu mazingira ambapo leo tutazungumzia utegemezi wa Afrika kwa kuni na taathira mbaya kwa misitu ya bara hilo kutokana na mahitaji makubwa ya makaa. Radionovela leo itawaeleza juu ya hatua mbadala zinazopatikana kukabiliana na hali hiyo. Je unajua kwamba inawezekana kupika chakula kwa kutumia ujoto na mwanga wa jua? Kadhalika tutaangalia jinsi uharibifu wa misitu yetu unavyobadili mienendo ya hali ya hewa na vipi misitu ya eneo la joto inavyofanya kazi kama sponji kubwa kabisa la kunyonya maji lakini miti hiyo inapokatwa kwa haraka sana ardhi inageuka kuwa kavu na jangwa lililo kame.

**Music – 0 : 30**

**SFX Birdsong + SFX – Approaching Footsteps ....Sauti ya ndege na hatua za miguu zinazokaribia**

**Moses:** Shikamoo Mama...

**Bibi.Tekwula:** Marhaba... Moses... aaah mwanangu umekaa tu badala ya kunisaidia kubeba hizi kuni... hebu inuka hapo!

**SFX Woodpiles hit Ground .....mzigo wa kuni uaanguka chini**

**Bibi Tekwula:** (catching her breath .....akipumuwa) Ehhhh! kwa ukongwe huu nilionao siwezi tena kuendelea kubeba kuni kutoka masafa marefu... tena kila siku... naona mwili karibu utanigomea.

**Monica:** Huwa unatembea umbali gani Bibi Twekula ?

**Bibi Tweekula** (claps her hands .....akipiga makofi) Ahhhh Monica  
...ni mbali sana kupindukia mlimani ....nyuma ya  
nyumba.

**Gladys:** Kwani huchukua muda mrefu ?

**Bibi Tweekula:** Saa moja kwenda na saa moja kurudi! Hebu fikiria  
Gladys... unatumia masaa mawili ya siku yako kwa  
ajili ya kutafuta kuni tu za kupikia. Natumai wakati  
nyinyi wasichana mtapozeeka kutakuwepo na umeme  
kwa kila nyumba na majiko ya kisasa yatakayokuwa  
rahisi kwa mtu kumudu kuyamiliki. Je kuna mtu  
anayehitaji chai?

**X –fade into SFX Small fire .....changanya na sauti ya moto  
mdogo**

**Moses:** Wakati nilipokuwa kijana mdogo mama nakumbuka  
ulikuwa huchukui muda mrefu kwenda kukusanya  
kuni ... pengine nusu saa tu...

**SFX Snapping Wood .....kuni zikidata....**

**Bibi Tekwula:** Kwa sababu ilikuwa ni rahisi kutafuta kuni. Eneo lote  
karibu na nyumba kulikuwa na miti na vichaka  
vidogo.

**Moses:** Na kulikuwa na msitu juu kule mlimani.

**Gladys:** Kwani msitu huo haupo tena Bibi Tweekula ?

**Bibi Tweekula:** Haupo tena Gladys. Miaka mitano iliopita msitu huo  
ulisafishwa kwa ajili ya kuanzisha shamba jipya...  
sasa kile kilichoko pale ni machungo ya ng'ombe.

**Monica:** Mnajua pale tunapoishi sisi hali ni kama hiyo.  
Kulikuwa na miti kila mahala lakini ikaanza  
kutoweka taratibu. Hali hiyo ilizidi kuwa mbaya pale

baadhi ya wanawake wa kienyeji waliposhajiishwa kutengeneza makaa kwa ajili ya kujipatia vijisenti kidogo.

**Gladys:** Nimesikia wakati nikiwa shuleni kwamba eneo la kusini mwa jangwa la Sahara barani Afrika misitu mingi inatumika kwa ajili ya kuni na makaa kuliko mahala popote pale duniani kwa kuzingatia tawkwimu za matumizi ya kila mtu mmoja.

### **SFX Stirring Tea.....Koroga Chai....**

**Bibi Twekula:** Eeh... eeh... mbona sio nzuri!

**Moses:** Lakini inakuwaje tunakuwa na matumizi makubwa sana kiasi hicho kwa kulinganishwa na wengine?

**Gladys:** Kwa sababu tuko tegemezi sana kwa misitu kama chanzo cha nishati.

**Monica:** Kwa kuongezea hapo Gladys idadi ya watu barani kote Afrika inaongezeka kwa haraka sana. Na hiyo ina maana kwamba sote huwa tunagombania rasimali moja. Kwahiyo sio kitu cha kushangaza Bibi Twekula kwamba inabidi tutembe masafa marefu sana kutafuta kuni zetu kwa sababu hakuna kuni za kumtosheleza kila mtu!

**Gladys:** Hebu jaribu kufikiria ingelikuwa sote tuna umeme kungelikuwa hakuna haja kwa wanawake kutumia masaa mengi kila siku kwa ajili ya kutafuta kuni na badala yake wangeliweza kutumia muda huo kujipatia fedha kwa shughuli nyingine.

**Bibi Twekula:** Na Monica unajuwa kitu kengine kilichokuwa tofauti hivi sasa... ni hali ya hewa! Nimekuwa nikiishi hapa maisha yangu yote na nakumbuka wakati nikiwa

msichana mdogo tulikuwa na majira ya mvua yanayotambulika kinaga ubaga.

**Gladys:** Mama yangu alikuwa akisema hayo hayo.

**Bibi Twekula:** Na kama matokeo basi... tulikuwa tukijua hasa wakati gani wa kupanda mazao yetu na wakati gani hasa tutakuwa tunavuna! Lakini hivi sasa fikra hiyo haiko tena kwani unaweza ukaotesha mbegu zako na siku ya pili ukashtukia zimesombwa na mvua!  
(sounding resigned .....akionyesha kuvunjika moyo)

**Moses:** Hebu twende tukanyoshe miguu... nataka niwaonyeshe mahala iliokuwepo misitu hapo zamani...

**X - fade SFX Small Fire into SFX Birdsong ... changanya sauti ya moto mdogo na ile ya ndege...**

**SFX – Cattle .....Ng’ombe**

**Moses:** (Kicking the dusting soil ....akipiga miguu yake chini katika udongo uliojaa vumbi ) Unaona udongo ulivyokuwa hivi sasa... zamani ulikuwa wa rangi nyekundu iliokoza... ulionekana kuwa na rutuba sana. Sasa unageuka kuwa vumbi tupu!

**SFX – Approching vehicle... sauti ya gari linalokaribia kufika...**

**Moses:** Shikamoo Bwana...

**James:** Marahaba! Jia langu ni James na ninafanya kazi na shirika moja la kienyeji la kutunza mazingira.

**Moses:** Karibu Bw. James. Mimi naitwa Moses.

**Gladys:** Mimi ni Gladys.

- Monica:** ...na mimi jina langu ni Monica.
- Moses:** Ndio sijui tukusaidie nini...
- James:** Mimi kilichonifikisha hapa hasa ni kutaka kuwashajiisha watu kuwacha kutumia kuni kwa ajili ya kupikia.
- Gladys:** Kama utatuamini hivi punde tu tulikuwa tukizungumzia juu ya ukataji wa misitu katika eneo hili.
- James:** Hali ni mbaya eenh.... au sio.Hivi sasa kumekuwepo na kilimo cha kupindukia kwenye milima na bila ya shaka kuna mahitaji ya kuni.
- Moses:** Ningelipenda kujuwa kwa nini udongo hivi sasa umekuwa na vumbi mno?
- James:** Unajuwa mizizi ya miti husaidia kushikamanisha sehemu ya juu ya udongo yenye virutubishi vya rutuba.Unapokata misitu hiyo hapo tena kunakuwa hakuna kitu cha kushikilia pamoja udongo huo.Wakati mvua inaponyesha sehemu ya juu ya udongo huwa rahisi kusombwa na maji hadi chini milimani.Udongo unaobakia unakuwa hauna rutuba sana.
- Monica:** Na Bibi Twekula mama yake Moses alikuwa akituambia kwamba mienendo ya mvua inabadilika.
- Moses:** Lakini kwa nini inakuwa hivyo?
- James:** Ndio ....jibu ni kwamba misitu huwa inafanya kazi ya kuwa kama spongi kubwa sana na wakati mvua inaponyesha hunyonya maji yake na baadaye baadhi ya maji hayo hunywewa na kurudi tena hewani katika utaratibu unaojulikana kama wa kutowa mvuke.Hii

husababisha kuwepo kwa mawingu na kwa hiyo mvua zaidi hunyesha tena.

**Gladys:** Kwa hiyo kuna hatua zozote vitu nyengine... za mbadala kukabiliana na hali hiyo?

**James:** Ndio Gladys kuna vitu mbadala vya aina mbali mbali hata kwa watu ambao hawana umeme.

**Moses:** Unaweza ukatupa mfano...

**James:** Kwanza ni jiko la mafuta lililofanyiwa marekebisho lakini litakuwa linachoma kuni.

**Monica:** Ehhh kuni tena! Sasa hapo kuna kitu kilichoboreshwa kweli?

**James:** Jibu hapo ni ndio na hapana. Majiko hayo bado yatakuwa yanahitaji kuni lakini kazi yake inakuwa ya ufanisi zaidi kuliko yale ya kienyeji yanayotumia kuni tupu uwanjani. Kwa kweli tunaamini baadhi ya majiko hayo yanakuwa na ufanisi wa zaidi ya asilimia hamsini. Kwa maneno mengine unakuwa unahitaji nusu tu ya kuni unazotumia kila wiki.

**Moses:** Na kuna vifaa vingine mbadala vya ziada ?

**James:** Ndiyo wacha niwaonyeshe... nina kifaa kimoja nimekiweka nyuma ya gari.

### **SFX Open Vehicle Door + SFX Pulling Out Metal Object ... Kufunguwa Mlango wa Gari + Kutowa nje Kitu cha Chuma**

**Monica:** Kitu gani hicho?

**James:** Hili Monica tunaliita jiko lenye kutumia nguvu za jua.

**Monica:** Linaitwaje?

**James:** Nisikilizeni kwa makini. Hiki ni kifaa ambacho hupika chakula kwa kutumia mwanga wa jua tu. Na kwa sababu hakitumii mafuta kinakuwa hakina gharama yoyote ile ya kukiendesha na kinasaidia kupunguza kasi ya ukataji wa misitu.

**Moses:** Kinaonekana kama... aina fulani ya dude kutoka anga za juu.

**James:** (Laughs .....anacheka ) Kwa kweli kuna aina mbali mbali za majiko ya kutumia nguvu za jua lakini yote yanazingatia fikra moja... nayo ni kwamba unapika chakula chako kwa kutumia ujoto na mwanga wa jua tu.

(collective ooooh.....sauti ya pamoja )

**James:** Hasa jiko hili huwa linakusanya mwanga na ujoto kutoka kwenye jua na kuuingiza kwenye kaeneo kadogo cha kupikia ndani ya jiko hili. Na kwenye eneo hilo la kupikia ndipo unapoweka sufuria yako.

**Gladys:** Na huwa linapika chakula kama vile katika moto wa kawaida au jiko linalohimili joto...

**James:** Linaweza kuhimili hali ya ujoto wa hadi nyuzi joto 150 za Selsiasi bila ya kupoa. Haliwi moto kama jiko la kawaida lakini bado linakuwa na moto wa kutosha kuweza kupika chakula kwa muda mrefu.

**Moses:** (Laughing .....Akicheka ) Sina uhakika sana mama yangu atasemaje juu ya jiko hilo...

**James:** Kama ni hivyo tusipoteze wakati... twendeni tutayajua huko mbele!

**Music: 0:30**

## **Je ulikuwa ukijua?**

Je ulikuwa ukijua kwamba misitu ilikuwa inafanya kazi kama maspongi makubwa? Huloanishwa na mvua inayoletwa na vimbuga vya joto wakati huo huo huwa nanga ya kushikamanisha udongo na kutowa maji kila baada ya vipindi fulani vya mapumziko. Kwa maana hiyo hufanya kazi kama mabwawa ya kuhifadhia maji. Misitu ya joto hapatikana kwenye maeneo unakopita mstari wa kati wa dunia Equator na huunda mzingo wa kuzunguka dunia. Hupata kima kikubwa sana cha mvua cha takriban centimeta 200 kwa mwaka na kutoka baadhi ya maeneo hufikia hata sentimita 100. Kile kinachoonekana kama kitu cha maajabu ni kwamba misitu hiyo ya joto huzalisha mvua yake yenyewe yaani kwa kweli hadi asilimia 75 ya mvua zinazonyesha kwenye misitu ya joto ni zile zinazozalishwa na misitu hiyo yenyewe.

Hapa tunafafanua zaidi jinsi hali hiyo inavyokuwa: Wakati mvua zinaponyesha juu ya misitu ya joto ile inayoweza kufika kwenye ardhi ya misitu hiyo kwa kweli inakuwa ni kidogo sana. Karibu mvua yote inakuwa inadukizwa na vipaa vinavyonin'ginia vya misitu hiyo. Baadhi ya maji ya mvua hiyo hutumiwa na miti na mengine hurudishwa kwenye udongo na hatimae katika mito na vijito vidogo. Lakini katika misitu ya maeneo ya joto duniani karibu asilimia hamsini ya maji hayo hurudishwa tena hewani kwa kupitia utaratibu unaojulikana kama wa kutowa mvuke. Hii ndio sababu misitu ya joto inakuwa ni mahala penye unyevu nyevu mkubwa. Maji ya unyevu huo baadae hufanya mawingu ya mvua ambayo hunyesha tena kama mvua.

Kwa hiyo nini kinatokea wakati misitu hiyo inapokatwa? Kunakuwa na unyevu kidogo unaorudishwa tena katika angahewa na kama matokeo kunakuwa na mawingu machache ya mvua na kwa hiyo kunakuwepo na upungufu wa mvua. Iwapo mvua inasita kunyesha hapo tena katika kipindi cha miaka michache tu eneo hilo linageuka kuwa kavu sana huku jua kali la maeneo ya joto likipiga ardhi ya pori hilo. Mfano mzuri wa hali hii ni kisiwa cha Madagascar barani Afrika.



Madagascar hapo zamani ilikuwa imefunikwa na kichaka cha misitu ya joto. Lakini hivi sasa pungufu ya asilimia 10 ya misitu ya joto ndio iliobakia kwenye kisiwa hicho na kwa kiasi kikubwa kisiwa hicho kimegeuka kuwa jangwa jekundu lisilokuwa na miti.

Misitu ya Afrika imefunika eneo la zaidi ya hekta milioni 800 na hufanya kama asilimia 17 ya misitu duniani. Lakini kima hiki ni kiduchu tu ikilinganisha na kima cha misitu iliokuwapo hapo zamani. Kwa mfano huko Afrika magharibi asilimia 90 ya misitu ya asili ya eneo hilo imetoweka.

Misitu ya eneo la joto ina mfumo mkubwa kabisa wa ekolojia wa maisha ya viumbe hai kutegemeana. Lakini mkusanyiko wa mimea na wanyama hutegemea maji ambayo huhifadhiwa na misitu. Ukikata misitu hiyo jua kwamba bwawa la kuhifadhi maji nalo pia hukauka!

### **Outro ...Funga Kipindi.....**

Na hapo ndio tumefikia tamati ya kipindi chetu maalum cha Sikiliza na Ujifunze kuhusu mazingira ambapo leo hii kimeleka kuni na ukataji wa misitu. Kwa hiyo inafaa kuzingatia na kukumbuka kwamba misitu yetu ina thamani kubwa zaidi ziada tu ya kuwa chanzo cha kupatia kuni. Ni mahala penye mifumo ya ekolojia na mkondo wa maji isiothaminika. Asante kwa kuwa nasi! Iwapo ungelipenda kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaelezea marafiki zako tafadhali nenda kwenye tovuti yetu [www.dw-world.de/lbe](http://www.dw-world.de/lbe). Kwaheri.